JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA MUFINDI

Shule ya Sekondari Idetero,
S.L.P 11,
Mufindi.
30.11.2020.

Kumb. Na. HW/MUF/ISS/S3146/VOL.17
Ndg .....
.....

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI IDETERO WILAYA YA MUFINDI MKOA WA IRINGA MWAKA 2021

1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021 na unatakiwa kuripoti tarehe 04.01.2021 Jumatatu saa 1:30 asubuhi. Shule ya Sekondari Idetero ipo wilaya Mufindi, tarafa ya Ifwagi, kata ya Mtwango katika kijiji cha Mtwango. Shule ipo umbali wa kilomita 43 kusini mwa makao makuu ya Wilaya ya Mufindi. Usafiri wa gari ni wa noa kwa nauli ya shilingi 4000/=.

Shule ni ya kutwa na ni ya mchanganyiko wa wanafunzi wavulana na wasichana, kuanzia kidato cha kwanza mpaka cha nne. Masomo yanayofundishwa ni Uraia, Kiswahili, Kiingereza, Historia, Jiografia, Fizikia, Kemia, Baiolojia, na Hisabati.

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1. WAVULANA

- Suruali mbili (02): rangi ya kijivu moja (1) na suruali ya rangi ya bluu iliyokolezwa (dark blue) moja (01), suruali ziwe na malinda mawili, ziwe na turn up, na mguuni chini iwe inch 16-17. Suruali zilizobanwa chini hazitaruhusiwa kabisa.
- Mashati meupe mawili mikono mirefu.
- Viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili. Viatu viwe vyenye kamba na kisigino kifupi.
- Tai mbili rangi ya kijivu na bluu iliyokolezwa (dark blue).
- Soksi nyeupe jozi 2
- Sweta la bluu lenye mshono wa V kifuani lisilo na maandishi na lenye mikono mirefu.
- Mkandamweusi
- Track suit rangi ya bluu iliyokolezwa yenye mistari myeupe jozi moja na raba jozi moja kwaajili ya michezo.

WASICHANA

- Sketi mbili (02): sketi ndefu ya rangi ya bluu iliyokolezwa (dark blue) moja (01) na sketi ya rangi ya kijivu moja (01). Sketi iwe ndefu mpaka miguuni.
- Blauzi nyeupe mbili mikono mirefu.
- Tai mbili: rangi ya bluu iliyokolezwa moja na rangi ya kijivu moja.
- Viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili. Skuna na viatu vyenye kisigino kirefu haviruhusiwi. Viatu viwe vyenye kamba.
- Soksi nyeupe jozimbili.
- Sweta la bluu lenye mshono wa V kifuani lisilo na maandishi na lenye mikono mirefu.
- Track suit rangi ya bluu iliyokolezwa yenye mistari myeupe jozi moja na raba jozi moja kwaajili ya michezo.

Kwa wale watakaovaa hijabu ni lazima rangi ya hijabu ifanane na rangi ya sare ya shule mfano ingeweza kuwa nyeupe kama blauzi.

VIFAA VYA KUJIFUNZIA

- Madaftari tisa (09) counter book kuanzia Q02 na kuendelea na daftari ndogo (exclellent page 200) kwaajili ya (orientation course).
- Begi (hand bag) ndogo jeusi kwaajili ya kuwekea daftari na vifaa vingine vya masomo.
- Kamusi (Dictionary) ya kiingereza – kiswahili au kiingereza- kingereza.
- Mkebe wa hesabu mmoja (mathematical set 1)

NB: Ukaguzi wa sare na vifaa utafanyika ilikuhakikisha kila mwanafunzi ana sare na vifaa alivyoagizwa.

MAHITAJI MENGINE

Ndoo moja ya lita kumi
Kwanja moja / jembe moja

03. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa sheria na 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi yenye dhamana na Elimu nchini na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi ambayo yamefafanuliwa kwa maandishi katika Appendix A, B na C.

Karibu sana Shule ya Sekondari Idetero

.....
Mtove, T.M
Mkuu wa Shule.

APPENDIX A/

……
……
……

Mkuu wa Shule,
Shule ya Sekondari Idetero,
SLP 11,
Mufindi.

YAH: KUKUBARI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MGOLOLO
MWANAFUNZ_____KIDATO CHA _____MWAKA_____

1.Mimi ..... Mzazi/mlezi wa mwanafunzi aliyetajwa hapo juu, ninakiri kuwa nimeyaelewa maelezo yote (joining instruction) yaliyotolewa.
2. Ninakubari mwanangu aendelee na masomo, na nitatekeleza yote yale yanayonihusu kwa wakati wake, kama ilivyoagizwa katika maelezo ya kujiunga na shule hii.
3. Naahidi kumhudumia mtoto wangu kwa hali na mali ilikufikia malengo yake ya kujiunga na shule hiyo.
4. Naahidi kusimamia nidhamu na maendeleo yake muda wote awapo hapo shuleni.

JINA LA MZAZI/MLEZI……
SAHIHI YAKE……
Nambaya simu……

Mimi……ninakubari kwa hiari yangu kujiunga na shule hii,naahidi kuwa mtiifu wa sheria za shule, kuwa na nidhamu, kusoma kwa bidii, na kuwa mfano wa kuigwa kwa wanafunzi wenzangu ilinifikie malengo ya kujiunga na shule hii.

JINA LA MWANAFUNZI……
SAHIHI……

APPENDIX B:

JINA LA MWANAFUNZI..... SAHIHI.....

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI
SHULE YA SEKONDARI IDETERO
S.L.P 11 MUFINDI

SHERIA NA KANUNI ZA SHULE AMBAZO MWANAFUNZI ANATAKIWA KUZIFUATA

A. SHERIA

1. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla.

2. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.

3. Kushiriki kwa umakini kufanya maandalio ya jioni.

4. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.

5. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.

6. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.

7. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.

8. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na

9. Kutunza mali za umma.

Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha mwanafunzi kufukuzwa au kusimamishwa shule:

- Wizi
- Uasherati, ushoga, ulawiti na usagaji
- Ubakaji
- Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli n.k.
- Kupiga au kupigana
- Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- Kudharau Bendera ya Taifa.
- Kupata mimba
- Kuoa au kuolewa
- Kutoa mimba
- Kugoma, kuchochea, na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- Kukataa adhabu kwa makusudi
- Kumiliki simu ya mkononi.

B. MAHUDHURIO

i. Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa.

ii. Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria kazi zote za mikono.

iii. Mwanafunzi anatakiwa kufanya mambo yafuatayo:

(a)Kuandika nukuu (notes) zote.

(b) Kufanya mazoezi yote anayopewa na mwalimu.

(c) Kutunza madaftari yake vizuri.

iv. Mwanafunzi anatakiwa kuja muda uliopangwa, yaani **KUWAHI SHULENI KWENYE VIPINDI DARASANI**

v. Mwanafunzi anatakiwa kuwahi kwenye shughuli zote.

vi. Mwanafunzi anatakiwa kukimbia mara asikiapo wito wa kengele au anapoitwa na mwalimu au mtu yeyote anayemzidi umri.

C.UVAAJI WA SARE ZA SHULE

I. Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na sare ya shule wakati wote awapo shuleni.

II. Anatakiwa kuvaa sare wakati wote wa,

(a) Masomo darasani.

(b) Anapotoka nje ya shule kwa shuguli za kishule

(c) Mhadhara wa shule

(d) Anapokwenda hospitali

(e) Kwenye maandamano

III. Anatakiwa kuhakikisha kuwa sare yake ni safi wakati wote

D.MIPAKA

I. Mwanafunzi asitoke nje ya mipaka ya shule bila kibari maalumu.

II. Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea sehemuzifuatazo:

(a) Vilabu vya pombe

(b) Baa

(c) Nyumba za kulala wageni

(d) Majumba ya starehe

(e) Nyumba za walimu zisiwe za mazoea kwa mwanafunzi, epuka

MOTTO

Education is Liberation

VISION

Creativity, Discipline and Wisdom are first in this school so as:

i. To train pupils for national development

ii. To increase academic performance

MISSION

We struggle for Good Academic Performance.oi

.

.....

Mtove, T.M

Mkuu wa Shule

APPENDIX C

DAKTARI .....
HOSPITALI YA .....
S.L.P .....

FOMU YA KUPIMWA AFYA MWANAFUNZI.

Tafadhali tunaomba umpime mwanafunzi aliyetajwa hapo juu kwa gharama za mzazi wake, na uthibitishe kama ataweza kumudu masomo ya sekondari katika shule hii. Ni muhimu apimwe kabla ya kuja hapa.

.....
Mtove, T.M.
MKUU WA SHULE

Mkuu wa Shule,
Shule ya Sekondari Idetero,
S.L.P 11,
Mufindi.

YAH: MWANAFUNZI.....

Matokeo ya vipimo vya afya ya mwanafunzi aliyetajwa hapo juu.

1. Urine .....
2. Stool .....
3. BP .....
4. Pregnancy test .....
5. Spleen .....
6. Chest .....
7. Physical abnormality .....

Nathibitisha kuwa mwanafunzi huyu .....ataweza/hataweza kumudu masomo ya sekondari kwasababu .....
.....

JINA LA DAKTARI **SAHIHI/CHEO** **TAREHE**
..... **.....** .....